

**MAONESHU YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM
KATIKA SIKUKUU YA WAKULIMA
(NANE NANE) YALIYOFANYIKA KATIKA VIWANJA VYA JULIUS NYERERE
MJINI MOROGORO KUANZIA TAREHE 01 AGOSTI HADI 08 AGOSTI, 2016**



Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita, akiwa na watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Shirika la Masoko Kariakoo na Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam alipotembelea banda la maonesho la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.



Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Bibi Theresia Mbando (kulia) akiwa na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Bibi Sipora Liana, katika jengo la maonesho ya Nane Nane la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam lililopo mjini Morogoro



Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Bibi Sipora Liana (Katikati), akiwa na watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam wakati wa maonesho ya Nane Nane mjini Morogoro.



Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Bi. Moshi Ponera, akikabidhiwa Cheti cha Ushiriki katika maonesho ya Nane Nane kutoka kwa Katibu wa Jumuiya ya Wakulima Tanzania (TASO), Bw. Idi Mbonde.



Afisa Maendeleo ya Jamii Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Bi. Margareth Mazwile, akijibu maswali ya masista waliotembelea maonesho ya Halmashauri ya Jiji waliotaka kujua mipango ya Halmashauri kuhusu ujenzi wa vituo vipya vya mabasi yaendayo mikoani na nchi za jirani



Masista wanaoonekana katika picha hii pia walitembelea maonesho ya Shirika la Masoko Kariakoo wakati wa maonesho ya Nane Nane mjini Morogoro



Afisa Biashara wa Shirika la Masoko Kariakoo, Bi. Mwinga Luhoyo, akiwaelimisha wanafunzi kuhusu shughuli za shirika hilo wakati wa maonesho ya wakulima mjini Morogoro



Afisa Mazingira wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Bw. Richard Kishere, akiwaelimisha wanafunzi kuhusu utunzaji mazingira katika maeneo yanayowavutia watalii katika Jiji la Dar es Salaam.



Afisa Utalii wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Bi. Neema Kinyagu, akiwaelezea wanafunzi mjini Morogoro wakati wa maonesho ya Nane Nane mpango wa Halmashauri ya Jiji wa kukuza utalii katika Jiji la Dar es Salaam



Afisa Habari wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Bi. Beatha Singano, akitoa elimu kwa umma kuhusu vipindi vinavyorushwa na redio ya Halmashauri ya Jiji, City FM Radio (91.7 Mhz)



Mbunge wa Viti Maalum(CCM) Mkoa wa Morogoro, Dkt Jasmine Tiisweka (Kushoto) akisikiliza kutoka kwa Meneja Uwekezaji wa Shirika la Shirikika laMaendeleo la Dar es Salaam (DDC), Bw. Hiza Francis, aliyekuwa akielezea shughughuli zinazofanywa na Shirika hilo na mipango yake ya uwekezaji.